**DAWA>>Serikali imeendelea kuziba mianya ya dawa feki za mifugo kulinda wafugaji**

# Waziri ataja mkakati wa kulinda mifugo, wafugaji

Na MWANDISHI WETU

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amesema serikali inaendeleza jitihada za kudhibiti uingizaji holela na utengenezaji wa dawa 'feki' za mifugo ili kuwalinda wafugaji nchini.

Ndaki alibainisha hayo jana alipotembelea eneo la kampuni ya uzalishaji, usambazaji na uingizaji wa pembejeo za mifugo na kilimo (Farmbase) lililopo wilayani Kigamboni, Dar es Salaam ambalo wanataka kujenga kiwanda kikubwa cha kuzalisha dawa za mifugo nchini.

"Hivi karibuni tuna mpango wa kuweka maduka ya kuuza dawa katika kila mnada ili kuwahakikishia wafugaji wetu kwamba dawa aliyonunua kutoka katika maduka hayo ni sahihi kuitumia, mpango wetu haya maduka yaendeshwe na watu binafsi chini ya usimamizi wa serikali," alisema.

Alisema kumekuwapo na malalamiko kutoka kwa wafugaji dhidi ya baadhi ya dawa wanazozitumia kutibu mifugo kutowapa matokeo wanayoyatarajia, ndio maana serikali inaendelea kudhibiti uuzwaji holela wa dawa hizo na kuimarisha utaratibu mzuri wa upatikanaji wa dawa halisi za mifugo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Farmbase, Suleiman Msellem alisema kuwa, kampuni hiyo ipo tayari kushirikiana na serikali katika kuhakikisha dawa zenye kukidhi vigezo na viwango kwa ajili ya mifugo zinapatikana kwa wingi nchini.

"Njia moja ya kuondosha dawa feki ni kupatikana kwa dawa halisi, sisi tupo tayari kushirikiana na serikali yetu, hata hayo maduka yakianzishwa tupo tayari kushirikiana katika kuzisambaza dawa kwenye maduka hayo," alisema.

# Ripoti ya moto Soko la Mchikichini kukabidhiwa leo

NA REHEMA MAIGALA

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makala leo anakutana na uongozi wa wafanyabiashara na kamati ya ulinzi na usalama wa mkoa kupokea ripoti ya kamati ya kuchunguza chanzo cha kuungua kwa Soko la Mchikichini, Dar es Salaam.

Soko hilo liliteketea kwa moto Januari 16, mwaka huu na kusababisha hasara mbalimbali ikiwamo kuteketea kwa bidhaa za wafanyabiashara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Msemaji wa Wafanyabiashara wa soko hilo, Ismail Faisal, alisema ripoti hiyo ya kamati itatoa majibu yote yaliyokuwa yanahitajiwa na wafanyabiashara hao.

> **"Serikali haiwezi kutuangusha hata siku moja, tunajua soko bado lipo mkononi mwetu kilichokuwa kinasubiriwa ni kukamilika kwa ripoti tu.**

"Kesho (leo) ni siku ya muhimu kwa wafanyabiashara ili kujua mustakabali wote kuhusiana na kurudi katika soko lao kwa ajili ya kuendelea na shughuli zao za kawaida," alisema.

Faisal alisema kuungua kwa soko hilo kumewasababishia wafanyabiashara hao kukosa sehemu ya kufanyia shughuli zao.

Hata hivyo, Faisal alisema tayari Mkuu wa Mkoa ameshawahakikishia wafanyabiashara wa soko hilo kuwa lipo mikononi mwao.

"Serikali haiwezi kutuangusha hata siku moja, tunajua soko bado lipo mkononi mwetu kilichokuwa kinasubiriwa ni kukamilika kwa ripoti tu," alisema.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa alitoa siku saba kwa ajili ya kuchunguza chanzo cha moto huo.

Bashungwa alisema ni mara ya tatu sasa kwa soko hilo kuwaka moto, hivyo kuna umuhimu mkubwa wa kulifanyia uchunguzi ili kubaini chanzo chake.

**IBADA**



MAKAMU wa Rais Dk. Philip Mpango na mkewe Mboni, wakishiriki ibada ya Misa Takatifu Dominika ya Tatu ya Mwaka C , wa Kanisa katika Kanisa Kuu Katoliki la Bikira Maria Mshindaji, Jimbo la Kigoma, jana. (Picha na Ofisi ya Makamu wa Rais).

# Mbarawa ataka kuharakishwa ujenzi miundombinu Kagera

Na MWANDISHI WETU

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa, amesema kufanikiwa kwa miradi ya kiuchumi na uzalishaji katika Mkoa wa Kagera kutategemea kukamilika kwa haraka kwa miundombinu ya barabara na madaraja mkoani humo.

Profesa Mbarawa aliyasema hayo jana alipokagua ujenzi wa daraja la Kitengule lenye urefu wa mita 140 na barabara unganishi zenye urefu wa kilomita 18.

... biashara na kuongeza uzalishaji wa sukari katika kiwanda cha Kagera.

"Kutokana na kazi kubwa inayofanyika hapa ya ujenzi wa daraja na barabara ni dhahiri kutachangia uzalishaji mkubwa wa miwa na mazao mengine ya kilimo.

"Nakuagiza Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Mkoa wa Kagera kuanza usanifu wa barabara hii sehemu iliyobaki ya Kitengule-Bunazi Kilometa 24 ili ...

... sukari cha Kagera kwa kuwekeza katika miundombinu ya maji itakayokiwezesha kuongeza uzalishaji wa sukari nchini.

Naye, Meneja TANROADS Mkoa wa Kagera Mhandisi Yudas Msangi, alisema ujenzi wa daraja la Kitengule umesanifiwa kupitisha uzito wa tani 100 na kwa sasa umefikia asilimia 90 kukamilika.

Alieleza kuhusu barabara unganishi zenye urefu wa Kilometa 18 zinatarajiwa kukamilika Mei mwaka huu.

Kwa upande wake, ...

... Seif Seif, alisema ujenzi huo utakapokamilika utarahishisha uzalishaji wa sukari katika kiwanda hicho na kuibua fursa nyingi za ajira.

"Tumejipanga kuongeza ukubwa wa mashamba ili kutatua changamoto ya upungufu wa sukari nchini," alisema.

Alisema kwa sasa kiwanda hicho kinazalisha tani 94,000 za sukari, hiyo ni kutokana na kukamilika kwa miundombinu ambayo inatoa fursa ya kuongeza mashamba.

Aliongeza katika miaka mitatu ... kiwanda kimejipanga ...

... mwaka.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Prof. Makame Mbarawa yuko katika ziara ya siku tatu kukagua maendeleo ya miradi ya Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi na kuhamasisha wadau wa mbalimbali kuibua fursa za uchumi mkoani Kagera.

**MIUNDOMBINU**

**SERIKALI**

Imekuwa ikitekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika maeneo mengi ya nchi ikiwemo mkoa wa Kagera

Scanned with CamScanner

a ulikuwa ni asilimia 93.6

# na
# a

raja la Nne na

ka nihakikishe
nzi bora kwa
olojia ni kuwa
saidie watoto
na kasi hii ya
ani".
utekelezaji wa
na tija kubwa
nchi nzima
kulingana na
fundishaji hali
yingine kuwa
na nyingine

u wa Tabora
is Chemistry"
naofundisha
cha kwanza
hiyo". alisema
ka matokeo
liyotoka hivi
umefaulisha
.6 na mtihani
dato cha pili
ha ni asilimia



ya Detail
onyesho
lia ni Balozi wa
Wanyama Pori

## nya kazi

nyiwa kazi na
tambua kuwa
a imekuwa na
na.
niundombinu,
wazi mikakati
kuhakikisha
irikishi kwa
mazingira ya
wao unakuwa
ama.
kuwahudumia
mbalimbali
ya ardhi na
utatua suala
lo limekuwa
shule nyingi

# Sekta ya Kilimo, Ufugaji kupewa kipaumbele Gairo

**NA WARIOBA IGOMBE,** *GAIRO*

WANANCHI wilayani Gairo wanaotegemea kilimo, ufugaji na biashara kujiingizia kipato wameiomba serikali kutilia mkazo maendeleo ya sekta hizo katika bajeti ijayo ili wajikwamua na umaskini na kuondokana na hali ngumu ya maisha.

Wananchi hao waliyasema hayo jana mara baada ya kumalizika kwa kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Gairo, ambapo waliomba serikali iangalie sekta ya kilimo, mifugo na biashara kwa jicho cha tatu kwa kuwa ndiyo kiini kikubwa cha uchumi wao.

> **"Katika mwaka wa fedha ujao tunahitaji bajeti ambayo itakwenda kutatua changamoto za wananchi wenye kipato cha chini kwani mbali na kutukomboa kiuchimi pia Halmashauri yetu itapata mapato mengi**
>
> Bona Senyagwa, mkazi Gairo

Akizungumza kwa niaba ya wenzake, Festo Chilama, ambaye ni mkazi wa Gairo, alisema mbali na wananchi wengi kutegemea sekta ya kilimo na mifugo kujikwamua kiuchumi lakini bado kuna changamoto kadhaa zinazorudisha nyuma maendeleo ya wananchi wa Gairo.

"Wananchi wa hapa wana kipato cha wastani, wengi tunategemea kilimo, ufugaji pamoja na biashara kujipatia kipato, hivyo tunaiomba serikali kupitia Halmashauri kuhakikisha bajeti ijayo inasaidia kutatua changamoto zilizopo"alisema Chilama.

Chilama alisema ili kuhakikisha uchumi wa wananchi wa Gairo unaimarika sekta ya kilimo na mifugo inatakiwa kuangaliwa kwa jicho la kipekee ili kuweza kutatua changamoto zinazowakabili wananchi kwa kuwa zitasaidia kuongeza uzalishaji.

Naye, Bona Senyagwa alisema miongoni mwa vitu vinavyotakiwa kutazamwa katika sekta hizi ni pamoja na pembejeo kwani zimekuwa ni gharama kubwa kuliko mitaji ya mkulima lakini pia katika wilaya hiyo upatikanaji wake ni wa shida.

Senyagwa alisema kuwa endapo sekta ya kilimo, mifugo ikiwa ni pamoja na biashara itaboreshwa kwa kutengewa bajeti itakayokwenda kutatua changamoto zinazowakabili wahusika uchumi wa Halmashauri ya Gairo utapaa juu zaidi.

"Katika mwaka wa fedha ujao tunahitaji bajeti ambayo itakwenda kutatua changamoto za wananchi wenye kipato cha chini kwani mbali na kutukomboa kiuchimi pia Halmashauri yetu itapata mapato mengi"alisema Senyagwa.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Gairo, Rachael Nyangasi alisema katika mwaka ujao wa fedha watatenga bajeti itakayoakisi katika masuala yote muhimu katika wilaya hiyo ikiwemo sekta za kilimo na mifugo.

Wakati huo huo, Mkuu wa Wilaya ya Gairo, Jabir Makame alisema atahakikisha anasimamia vyema mipango yote imayohusu sekta hizo muhimu kwa wananchi ili kuweza kuleta tija zaidi katika suala zima la uzalishaji mali kwa manufaa ya wananchi na taifa.

Scanned with CamScanner

HABARI ZA BIASHARA

HABARI LEO UK 17.

# Utengenezaji holela dawa za mifugo kudhibitiwa

Na Mwandishi Maalumu

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amesema serikali inaendeleza jitihada za kudhibiti utengenezaji holela wa dawa za mifugo pamoja na dawa feki za mifugo zinazoingizwa nchini ili kuwalinda wafugaji.

Alisema hayo jana alipotembelea eneo la kampuni ya uzalishaji, usambazaji na uingizaji wa pembejeo za mifugo na kilimo (Farmbase) lililopo wilayani Kigamboni, Dar es Salaam ambako itajenga kiwanda kikubwa cha kuzalisha dawa za mifugo.

Alisema kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wafugaji kuwa kuna baadhi ya dawa wanazozitumia kutibu mifugo yao haziwapi matokeo wanayoyatarajia, ndio maana serikali inaendelea kudhibiti uuzwaji holela wa dawa hizo na kuimarisha utaratibu mzuri wa kupatikana dawa halisi za mifugo.

"Hivi karibuni tuna mpango wa kuweka maduka ya kuuza dawa katika kila mnada ili kuwahakikishia wafugaji wetu kwamba dawa anayonunua ni sahihi, mpango wetu haya maduka yaendeshwe na watu binafsi chini ya usimamizi wa serikali," alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Farmbase, Suleiman Msellem alisema wapo tayari kushirikiana na serikali kuhakikisha dawa halisi kwa ajili ya mifugo zinapatikana kwa wingi nchini.

# Stanbic yafungua tawi lililoungua Kariakoo

Na Mwandishi Wetu

BENKI ya Stanbic Tanzania imefungua upya tawi lake la Kariakoo, Dar es Salaam baada kuteketea katika janga la moto lililotokea Soko Kuu la Kariakoo.

Tawi jipya la benki hiyo sasa lipo Mtaa wa Narung'ombe na Sikukuu Kata ya Kariakoo.

Hafla ya uzinduzi wa tawi hilo ilihudhuriwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla akiwa mgeni rasmi.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Mtendaji Mkuu wa Stanbic Tanzania, Kevin Wingfield alisema hatua hiyo ya kimkakati inalenga kuendelea kuwahudumia wafanyabiashara waliopo Kariakoo na maeneo ya jirani.

"Tawi letu la Kariakoo limekuwepo kwa zaidi ya miaka 10. Tumechagua kubaki eneo la Kariakoo kwa sababu tunafahamu umuhimu wa mchango wa wafanyabiashara wa eneo hilo kwa uchumi wa taifa pamoja na nchi jirani," alisema.

Makalla aliipongeza benki hiyo kwa jitihada za kuhakikisha wakazi na wafanyabiashara wa Kariakoo wanapata huduma za kifedha kwa urahisi.

Naye, Mkuu wa Kitengo cha Wateja wa Rejareja wa Stanbic, Omari Mtiga alisema benki hiyo yenye historia kubwa ya kufanyakazi kwa zaidi ya miaka 25 nchini, ina utaalamu na uwezo wa kuchochea uwekezaji ndani ya Tanzania na kukuza uchumi wa Tanzania na nchi za jirani.




Katibu Mkuu wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Fatma Mbarouk Khamis (wa pili kulia) akibadilishana mkataba wa makubaliano ya ushirikiano na Ofisa Mkuu wa Biashara na Wateja binafsi wa benki ya NMB, Filibert Mponzi kwenye hafla iliyofanyika mjini Unguja jana. Wa pili kushoto ni Meneja wa NMB Tawi la Zanzibar ambaye pia ni Kaimu Meneja wa Biashara, Naima Shaame, Mkuu wa Biashara ya Kadi NMB Zanzibar, Philbert Cashir (kushoto) na Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Hafsa Mbamba (kulia). (Picha na NMB).

# Wizara ya Utalii Z'bar, NMB kuwafunda watembeza watalii

Na Mwandishi Wetu

WIZARA ya Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar kwa kushirikiana na benki ya NMB itatoa mafunzo kwa vijana wanaotembeza watalii ili kurasimisha shughuli zao waweze kukopesheka.

Hayo yalisemwa na Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Fatma Mabrouk Khamis wakati wa kutiliana saini makubaliano kati ya wizara hiyo na NMB ili kuinua shughuli za utalii Zanzibar.

Akizungumza wakati wa mkutano huo uliofanyika jana Zanzibar, Fatma alisema kuna kundi kubwa la vijana wanaozagaa mitaani bila ujuzi wa kuongoza watalii na kuharibu taswira ya visiwa hivyo, ambapo wakipewa mafunzo na kurasimishwa itawasaidia kiuchumi na kijamii na kuendesha shughuli zao kwa ufanisi.

"Vijana wanaojihusisha na utalii mfano 'Beach boys' mara nyingi wanakuwa kero kwa wageni, wanafanya utalii wa mikobani. Kwa kushirikiana na NMB tutawakusanya tutawapa mafunzo na kuangalia ni kwa namna gani tunaweza kuwaunga na jumuiya ili kuwarasimisha na kuwaongoza, kwasasa hakuna miongozo inayowasimamia," alisema.

Aidha, Fatma alisema pia makubaliano hayo yanahusisha kuboresha mashamba ya viungo ambayo vijana wanajihusisha na shughuli hizo. "Tutashirikiana na NMB kuwapa mafunzo na mikopo ili kuboresha bidhaa zao, tutawashika mkono ili kuhakikisha wanatoa huduma nzuri na bidhaa nzuri," alisema.

Ofisa Mkuu wa Biashara na Wateja Binafsi wa NMB, Filbert Mponzi alisema benki hiyo imekuwa ikifanya mambo mengi makubwa Zanzibar kwa lengo la kuinua sekta ya utalii, ndiyo maana wameamua kupeleka vituo vya mauzo 100 ambapo kwa sasa wanaiomba Wizara ya Utalii kuwaelekeza vituo watakaposambaza vifaa kwa ajili ya kufanyia malipo.

"NMB ndio benki kubwa zaidi nchini ambayo serikali ni mdau mkubwa, lakini pia inaongoza kwa kupata faida yaani kwa ukubwa, tunapoingia kwenye jukumu kama hili hatuna wasiwasi," alisema.

# Wajasiriamali nchini watakiwa kujifunza kwa Bakhresa, Mengi

Na Joseph Sabinus

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Wadau wa Nishati Jadidifu Tanzania (Tarea), Prosper Magali amewataka wajasiriamali nchini kujifunza kwa wafanyabiashara Salim Said Bhakresa na Reginald Mengi kuanzisha, kukuza na kuendeleza miradi na biashara.

Alitoa rai hiyo juzi katika uzinduzi wa kitabu chake kiitwacho 'Anza, kua na ustawi katika miradi na biashara: mbinu za kipekee za kuanzisha, kukuza na kuendeleza miradi na biashara,' Dar es Salaam juzi.

Kitabu hicho kimeandikwa na Magali ambaye ni Mkurugenzi wa Ubunifu na Uendelezaji Miradi wa Ensol (T) Limited inayotoa huduma za kihandisi katika sekta ya nishati ya jua.

Alisema Bakhresa na Mengi (marehemu) ni wafanyabiashara ambao walioanzia katika hatua ndogo na ngumu na kukabiliana na changamoto nyingi, lakini kwa kuzingatia bidii, nidhamu na uaminifu wamefikia hatua ya kuwa na kampuni kubwa na nyingi zinazotoa huduma kitaifa na kimataifa.

Alisema miongoni mwa mambo makubwa yanayoelezwa kwa kina katika kitabu hicho ambacho dibaji yake imeandikwa na Profesa Geoffrey John wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) ni pamoja na mbinu za kisasa za kuanzisha miradi pamoja na misingi ya mafanikio katika biashara na maisha.

Alisema mengine ni Azimio la Arusha na fura za ujasiriamali, umuhimu na mbinu za kupata na kutumia mikopo kwa manufaa ili kupata maendeleo, visingizio vinavyowafanya watu washindwe kuanzisha biashara au miradi, mbinu za kugeuza matatizo/ changamoto kuwa fursa na mbinu za kupunguza kiwango cha kodi bila kuvunja sheria za nchi.

"Watu wengi wanafikiria, wanatamani, wanapenda na wanataka kufanya ujasiriamali, lakini wanakosea katika kuanza, anza na ulicho nacho hata kama ni kidogo kisha kiwekee mikakati ikikue na kuongezeka," alisema Magali.

Kuhusu kukopa kwa usahihi, mwandishi huyo alisema: "Watu wengi waliofanikiwa waliwekeza katika rasilimali zisizohamishika kama ardhi na majengo, lakini wengi pia wanakosea kutafuta kuwekeza katika miji mikubwa pekee."

"Yaliyo katika kitabu hiki yakisomwa na kuzingatiwa yatatoa hamasa kwa watu wengi zaidi na kutoa msukumo mpya wa kufungua biashara, kuzimiliki na kuzifanya kuwa bora, endelee na zenye mafanikio."

Scanned with CamScanner

HABARI LEO UK 18.

# RC asifu uboreshaji mahakama mtandao

**Na Fadhili Abdallah, Kigoma**

MKUU wa Mkoa Kigoma, Thobias Andengenye amewataka watumishi na watendaji wa mahakama kujipanga vizuri kuendana na maboresho makubwa yaliyofanywa katika utoaji huduma za mahakama mtandao.

Andengenye amesema hayo mjini Kigoma jana wakati wa uzinduzi wa wiki ya shughuli za mahakama.

Alisema kuwa maboresho makubwa ya utendaji wa mahakama ni maendeleo makubwa katika upatikanaji wa haki kwa jamii.

Alisema kuwa maboresho na maendeleo makubwa ya utendaji wa mifumo ya utoaji haki inaweza isiwe na maana kama watendaji hawatendaana

# Machinjio Nguru Hills kuanza kazi leo

**Na John Nditi, Morogoro**

MACHINJIO ya kisasa ya Nguru Hills yenye uwezo wa kuchinja ngombe 100,mbuzi na kongoo 2,000 kwa siku yanatarajia kuanza rasmi Machi Mosi, mwaka huu.

Machinjio hayo yaliyoko Mvomero mkoa wa Morogoro yanatarajia kuchochea ukuaji wa uchumi na ajira.

Mradi huo wa ubia kati ya Serikali kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa watumishi wa Umma(PSSSF ), Eclipse Investiment (LLC) na Kampuni ya Busara Innvestiment (LLP) ulioanzwa kutekelezwa mwaka 2018 lakini ugonjwa Covid- 19 ulisababisha kuchelewa kuzinduliwa.;

Mkurugenzi wa Mipango na Uwekezaji wa PSSSF , Fortunatus Magambo alisema hayo juzi mbele ya wahariri wa kutoka vyombo mbalimbali vya habari nchini waliofanya ziara ya kutembelea na kujionea maendeleo ya mradi wa machinjio hayo ya kisasa ya Nguru Hills Ranch Ltd.

Kuchelewa kwake kulisababisha na mashine zilizoagizwa kutoka nje kuchelewa kuletwa wakiwemo wataalamu wake. Mashine hizo hata hivyo zilifika Julai mwaka jana na kuanza kufungwa.

Magambo alisema, tayari mifumo ya maji , umeme , ufungaji wa mashine za kuchinjia na mifumo ya kupoozea vyote vimekamilika kwa asilimia kubwa zaidi .

Machinjio hayo yataajiri wafanyakazi 300 kwa hatua ya awali na miongoni mwao 120 watakuwa ni wa kudumu.

" Tupo katika hatua ya mwisho hapa kila kitu kimeisha , tutakachofanya kuanzia leo tutaanza kuleta ng'ombe wa kunenepesha kwa ajili ya kuchinja " alisema Magambo

Magambo alisema, machinjio hayo yatakuwa na uwezo wa kutunza ng'ombe 10,000 kwa mara moja na kwa siku ngo'mbe 100 watakuwa wakichinjwa pamoja na mbuzi 1,000.

Alisema soko kubwa la nyama itakayozalishwa itakuwa la nje ya nchi kwa asilimia 80 hususani nchi za mashariki ya kati kwa maana Uarabuni na asilimia zilizobaki zitakuwa kwa ajili ya soko la ndani.

Mkurugenzi wa Mipango na Uwekezaji alisema, mradi utaongeza kipato cha wakulima,kwa kununua mazao ambayo yatatumika kutengeneza chakula cha mifugo kwa ajili ya kunenepesha mifugo kabla ya kuchinja.

Naye Meneja Uhusiano na Elimu kwa wanachama wa Mfuko huo, James Mlowe alisema fedha iliyowekwa na Mfuko huo wenye hisa asilimia 39 ni Dola za Kimerekani milioni 3.9 sawa na fedha za Kitanzania takribani bilioni 8. 9.



# Mwanasiasa John nchimbi afariki dunia

**Na Mwandishi Wetu**

MWANASIASA mkongwe nchini John Nchimbi amefariki jana wakati akitibiwa taasisi ya moyo ya Jakaya Kikwete, mkoani Dar es Salaam .

Katika taarifa iliyotolewa na Katibu wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Itikadi na Uenezi na Chama, Shaka Hamdu Shaka imesema Chama hicho kimepokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kifo mkongwe huyo.

Aidha Chama Cha Mapinduzi kimetoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki kwa msiba huu mzito na kuwaomba kuwa na moyo wa subira katika kipindi hiki kigumu cha maombolezo.

"Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ndugu Samia

Scanned with CamScanner

# *Kibano kwa viwanda bubu vya dawa za mifugo*

Na Mbaraka Kambona

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amesema serikali inaendeleza jitihada za kudhibiti utengenezaji holela wa dawa za mifugo na zisizokidhi viwango za mifugo zinazoingizwa, ili kuwalinda wafugaji nchini.

Waziri Ndaki alibainisha hayo jana alipotembelea eneo la Kampuni ya Uzalishaji, Usambazaji na Uingizaji wa pembejeo za mifugo na Kilimo (Farmbase) lililoko wilayani Kigamboni, mkoani Dar es Salaam ambalo wanataka kujenga kiwanda kikubwa cha kuzalisha dawa za mifugo.

Alisema kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wafugaji kuwa kuna baadhi ya dawa wanazozitumia kutibu mifugo yao haziwapi matokeo wanayoyatarajia, na ndio maana serikali inaendelea kudhibiti uuzwaji holela wa dawa hizo na kuimarisha utaratibu mzuri wa kupatikana dawa halisi za mifugo.

"Hivi karibuni tuna mpango wa kuweka maduka ya kuuza dawa katika kila mnada ili kuwahakikishia wafugaji wetu kwamba dawa aliyonunua kutoka katika maduka hayo ni sahihi kuitumia, mpango wetu haya maduka yaendeshwe na watu binafsi chini ya usimamizi wa serikali," alisema Ndaki

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Farmbase, Suleiman Msellem, alisema kuwa wao wapo tayari kushirikiana na serikali katika kuhakikisha dawa halisi kwa ajili ya mifugo zinapatikana kwa wingi nchini.

"Njia moja ya kuondosha dawa feki ni kupatikana kwa dawa halisi, sisi tupo tayari kushirikiana na serikali yetu, na hata hayo maduka yakianzishwa tupo tayari kushirikiana katika kuzisambaza dawa kwenye maduka hayo," alisema Msellem.

## Benki ya Stanbic yazindua upya tawi lake la Kariakoo

Na Mwandishi Wetu

BENKI ya Stanbic Tanzania imefungua upya tawi lake la Kariakoo kufuatia janga la moto lililotokea katika soko la Kariakoo ambapo tawi la zamani liliathiriwa.

Taarifa ya benki hiyo ilieleza kuwa

Scanned with CamScanner

MWANANCHI UK 19.

VITA VYA UMASIKINI

# Wanufaika wa Tasaf wajenga nyumba bora

Peter Elias, Mwananchi
pelias@mwananchi.co.tz

Handeni. Wanufaika wengi wa Mpango wa kunusuru kaya masikini (Tasaf) wilayani hapa wamefanikiwa kujenga nyumba bora za makazi kupitia fedha wanazozipata kwenye mpango huo.

Wanufaika hao wameboresha maisha yao kupitia kushughuli ndogondogo wanazozifanya kama vile biashara na ufugaji ambazo wamezianzisha kwa kutumia fedha wanazopewa kwenye mpango wa Tasaf.

Wanaeleza kwamba kabla ya kunufaika na mpango, maisha yao yalikuwa magumu na walikuwa wakiishi kwenye nyumba za tembe lakini sasa wamefanikiwa kujenga nyumba za bati huku wakijishughulisha pia na ufugaji.

Mkazi wa Mtaa wa Kideleko, wilayani Handeni, Dorcas Mganga alisema tangu alipoanza kupokea Sh96,000 kutoka Tasaf, alikuwa akiweka kidogo kidogo kwa kununua matofali, bati na mbao hadi akakamilisha ujenzi.

Mratibu wa Tasaf - Handeni Mji, Frank Anania alisema walengwa wengi wa mpango huo wamefanikiwa kutatua changamoto ya makazi kwa sababu walikuwa wanaishi kwenye nyumba za tope na msimu wa mvua unapoanza wanapata shida ya kujisitiri.

**'Jambo la lazima ambalo huwa tunawaa mbia ni kwamba kama kuna mtoto nyumbani lazima ampeleke shule na kumnu nulia mahitaji yake kupitia fedha hizo. Hiyo imeongeza pia mahudhurio ya wanafunzi huko shuleni.'**

**Frank Ananaia**



Zainab Shaban, mkazi wa handeni akiwa amesimama kwenyejumba aliyojenga kwa msaada wa Tasaf. **Picha na Peter Elias**

## Waziri Ndaki alia na wakusanyaji wa maduhuli

Tuzo Mapunda, Mwananchi
tmapunda@mwananchi.co.tz

Dar es Salaam. Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amewataka wataalamu wa mifugo wanaohusika na ukusanyaji wa maduhuli kuwa waadilifu, waaminifu na wajitolee ili kufikia malengo yaliyowekwa.

Taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na wizara hiyo, ilieleza kuwa Ndaki alitoa maelekezo hayo katika kikao na wataalamu hao kilichofanyika juzi.

Ndaki alisema mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli mwaka 2021/2022 si mzuri akisema kati ya Sh50 bilioni zilizokusudiwa kukusanywa zilizopatikana hadi nusu mwaka ni Sh13.9 bilioni.

Kufuatia hali hiyo, aliwataka wataalamu hao kuhakikisha wanaacha alama ya ukusanyaji mzuri wa maduhuli ya Serikali katika kipindi chote cha utumishi wao.

Ndaki alimuelekeza katibu mkuu wa wizara hiyo, Tixon Nzunda kuwasiliana na katibu mkuu Tamisem kuhakikisha halmashauri zilizotumia fedha za maduhuli zikiwemo ya Mvomero, Tarime na Manyoni zinarejesha fedha hizo.

Kwa upande wake, Nzunda alisema wataalam hao watalazimika kuwajibika kutokana na matendo yao katika ukusanyaji wa mapato na kusisitiza waache tabia ya udanganyifu.

**Sh13.9 bil**

Fedha zilizokusanywa katika maduhuli ya Serikali katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi hadi nusu mwaka.

**Sh50 bil**

Malengo ya ukusanyaji maduhuli katika Wizara ya Mifugo mwaka 2021/2022.

Scanned with CamScanner

## Kwa Ufupi

### Pinda: Mauaji ya albino sitayasahau

**Dodoma.** Waziri Mkuu Mstaafu Mizengo Pinda amesema miongoni mwa vitu vinavyouumiza moyo wake ni mauaji ya watu wenye ualbino.

Kauli hiyo ameitoa juzi wakati akizungumza katika mkutano wa wa Amani wa Jumuiya ya Maridhiano Tanzania, ambapo alisema miaka miwili ya 2008/2009 ilikuwa migumu kwake akiwa Waziri Mkuu kutokana na kushamiri kwa mauaji hayo lakini alifaulu kupitia viongozi wa dini.

Pinda alishawahi kumwaga chozi wakati akijibu swali la papo kwa hapo bungeni lililouliza kuhusu mauaji ya wenye ualbino na aliamua kushirikiana na mkewe (Tunu) kulea kulea vijana wenye ualbino.

**Sharon Sauwa**

### Orodha makandarasi wabovu kuandaliwa

**Njombe.** Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (Tarura) mhandisi Victor Seff ameagizwa kuwaorodhesha makandarasi wote wenye rekodi ya kufanya vibaya ili wafutiwe leseni ya kufanya kazi nchi nzima.

Agizo hilo limetolewa jana na Waziri wa Nchi(Tamisemi), Innocent Bashungwa wakati akikagua barabara ya Igosi - Ujindile Wangama yenye urefu wa kilomita 16.9 iliyopo wilayani Wanging'ombe mkoani Njombe.

Naye Meneja wa Tarura, Wilaya ya Wanging'ombe Boniface Kasambo ujenzi wa barabara utasaidia wakazi wa wilaya hiyo kusafiri-

## UWEKEZAJI

Wahariri wa vyombo vya habari nchini wakimsikiliza Meneja wa kiwanda kusindika nyama cha Nguru Hills cha wilayani Mvomero mkoani Morogoro, Paul Felix alipokuwa akitoa maelezo juu ya maendeleo ya ufungaji wa mashine katika kiwanda hicho. Picha Lilian Lucas



BIASHARA

# Kiwanda cha nyama kuanza Machi

> **"Wanachama wasiwe na hofu ya fedha zao kwakuwa sisi tunawekeza kwenye maeneo ambayo fedha iko salama."**
> Fortunatus Magambo

Lilian Lucas,Mwananchi - llucas@mwananchi.co.tz

**Morogoro.** Kiwanda cha kusindika Nyama cha Ngulu Hills kilichoko wilayani Mvomero, mkoani Morogoro, kinatarajia kuanza uzalishaji wake Mwezi Machi mwaka huu baada ya kukamilika ufungaji wa mitambo na mashine za kuchinja mifugo na kusindika nyama.

Akizungumza na waandishi wa habari kiwandani hapo, mara baada ya wanachama wa Jukwaa la wahariri Tanzania (TEF) kutembelea kiwanda hicho, Mkurugenzi Mipango na Uwekezaji wa mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) Fortunatus Magambo, alisema wamewekeza Sh9 bilioni katika kiwanda hicho na tayari wana soko la ndani na nje ya nchi.

Magambo alisema mradi huo wa uwekezaji ulianza 2018 lakini kutokana na kuibuka kwa wimbi la Uviko-19 mashine zilichelewa kufika nchini na baada ya kufika wataalamu nao waliwasili Julai 2020 na walianza kufunga mashine na sasa wako katika hatua za mwisho.

Mkurugenzi hiyo alisema wakati wowote kuanzia sasa ng'ombe wataanza kununuliwa na kupelekwa ili wanenepeshwe kwa ajili ya maandalizi ya kuchinjwa kuanzia Machi 1,2022 Alisema wanatarajia kuajiri wafanyakazi zaidi ya 300 lakini kwa kuanzia watatoa ajira 120 za moja kwa moja lakini pia kiwanda kitakuwa na uwezo wa kuzalisha kazi nyingine.

"Pindi tutakapoanza uzalishaji, kiwanda kitakuwa na uwezo wa kuchinja Ng'ombe 100 kwa siku," alisema Mkurugenzi Magambo.

Naye Mjumbe wa Kamati Utendaji wa TF, Salim Said Salim alisema uwekezaji huo ni kwa manufaa ya wananchi na wanachama wa mfuko husika ambapo sasa wana uhakika wa fedha walizowekeza.

Alisema kiwanda hicho kitatoa ajira za muda mfupi na mrefu na wahariri wana jukumu la kuelimisha umma na wanachama wa PSSSF juu ya umuhimu wa uwekezaji huo kwa ataifa na maisha ya mtu mmoja mmoja.

Meneja Uhusiano na Elimu kwa wanachama James Mlowe alisema kuwa tangu kuanza kwa mfuko wa PSSSF miaka mitatu iliyopita mfuko umefanikiwa kulipa mafao ya zaidi ya Sh6. 4 trilioni kwa wanufaika 178,000

za kuchochea na kukuza maendeleo ya kiuchumi kwa mtu mmoja mmoja na jamii kwa ujumla.

Naye mhandisi mkazi wa mradi huo Zuber Magazini alisema maandalizi na utunzaji wa mazingira unaendelea vizuri.

Scanned with CamScanner